

- Kilo nane za *Leucaena*, *Gliricidia*, *Clitoria* au *Mucuna*, ambao haujakaika au kilo mbili za mimea hiyo kama imekauka na gramu sitini za maclick super kama malisho ya kuboresha.

Wape mifugo maji safi wakati wote.



Ng'ombe wakila vipande vya mihogo



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax. 254-20-4183344

Barua pepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Watayarishaji:

Kiura J.N., S Bimbuzi., Mwakina D. na Furaha

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkuu wa Kituo,

KARI-Mtwapa

S.L.P. 16, Mtwapa

Simu: 041-485842/5486207/0202024751

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 51 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Kutayarisha mizizi ya mihogo kuwalisha ng'ombe



Utangulizi

Utumiaji wa mihogo katika malisho ya mifugo haujatumiwa kadri inavyofaa. Aina ya mihogo iliyoimarishwa yaweza kutoa tani 30 za mizizi kwa kila hekari. Mizizi ya ziada na ile isiyofaa sokoni inaweza kutumiwa kama lishe ya mifugo.

Kuandaa mizizi ya mhogo kwa kuikausha inasaidia uhifadhi na kupunguza sumu.


Jinsi ya kuandaa mhogo

Hatua ya kwanza: Kuosha na kukatkata

- Osha mizizi ya mihogo baada ya kuvuna ili kutoa udongo.
- Katakata mizizi vipande-vipande kiasi cha mbegu ya mahindi au zaidi kidogo. Panga au mashine ya mkono yaweza kutumika.



Mihogo inakatwakatwa kwa mkono




Mihogo ikikahwakahwa na mashine

Hatua ya pili: kukausha


Siku ya nne, toa hizi vipande na na uvihifadhi kwenye gunia la makonge. Kutoka kilo 100 za mihogo huenda ukatoa kilo 28 za vipande kavu vya mihogo. Tandaza vipande kwa karatasi ya nailoni juu ya vitanda vya kukaushia vilivyinuliwa ili kuepuka maradhi yanayotoka mchangani.

Vipande vya nailoni pia hutumiwa pia kwa kufunikia vipande vya mihogo usiku au mchana kama kunanyesha.

Geuza vipande vya mihogo vilivyo kwenye kitanda cha kukaushia mara nne kwa siku ili kuharakisha ukaushaji na kuzuia viini (mould) kumea.



Vipande vya mihogo kwa kitanda cha kukaushia



Vipande vilivyokaushia kwenye mifuko

Mazao

Mizizi inayotoka punde tu hutoa tani 30 kwa kila hekari. Kilo 4,550 za mhogo uliokaushwa zinaweza kupatikana baada ya kuandaa ni zinaweza kulisha ng'ombe saba kwa mwaka. Kiasi hiki cha vipande vya mihogo kina uwezo sambamba kwa kuimarisha ukuzaji maziwa wa kilo 7,292 za mahindi ambacho hugharimu shilingi 62,400. Hiki ndicho kiasi cha fedha ambacho mkulima huhifadhi kwa kutumia vipande vya mihogo.

Malisho

Ng'ombe wastani anaweza kulishwa ifuatavyo kwa siku:

- Mpe nyasi ya Napier, silage au hay hadi ashibe.
- Kilo tatuza mihogo ilivyokaushwa ikiwa imegawa kwenye vipande vitatu sawa na kulishwa mifugo nyakati tofauti.